**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

SCHOOL BASED ASSESSMENT

# KISWAHILI SEHEMU A

Gredi ya 7

# NAKALA YA MWALIMU

**SEPTEMBA 2024**

**Geuza ukurasa**



@ KNEC 2024

**Sehemu A inatathmini Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza. Inajumuisha mazoezi matatu:**

i. Mazungumzo ya ana kwa ana

ii. Ufahamu wa Kusikiliza

iii. Kusoma kwa sauti

**MUDA: Dakika 15 kwa kila mwanafunzi.**

**Maagizo ya jumla**

1. Mwalimu awafahamishe **wanafunzi wote** kwamba mazoezi yote katika sehemu hii yatakuwa tathmini ya ana kwa ana. Kila mwanafunzi atakuwa na zamu yake ya kutathminiwa; mmoja baada ya mwingine.
2. Mwalimu awafahamishe wanafunzi wote kwamba karatasi hii ina mazoezi matatu:
    i. **Mazungumzo ya ana kwa ana**
    ii. **Ufahamu wa Kusikiliza**
    iii. **Kusoma kwa Sauti**
3. Mwanafunzi aandaliwe kiti au dawati kutazamana na mwalimu.
4. Mwalimu atangulize kila zoezi na amfahamishe mwanafunzi matarajio ya kila zoezi.
5. Mwalimu amfahamishe mwanafunzi kukamilika kwa kila zoezi.
6. Mwalimu atathmini umilisi wa mwanafunzi kwa mujibu wa mwongozo wa kutathminia pamoja na kuweka rekodi.



@ KNEC 2024

**ZOEZI I: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

**( I ) MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA**

**Maagizo maalum**

i. *Andaa mazingira mazuri ya tathmini kwa kumkaribisha mwanafunzi.*

ii. *Mwamkue na kumwomba akae.*

iii. *Jitambulishe kwake kwa kusema, 'Mimi ni mwalimu________________'.*

iv. *Muulize jina lake.*

v. *Anza tathmini kwa kusema,*

"Ulimwengu wa sasa umeshuhudia kuzuka kwa magonjwa mbalimbali. Leo tutazungumza kuhusu magonjwa yanayoambukizwa.

1. Hebu nitajie ugonjwa wa kuambukizwa unaoufahamu?

   **(Mwanafunzi ajibu)**

2. Umegundua kwamba kijijini mwenu mna ongezeko la maambukizi ya kipindupindu. Utawawashauri wanakijiji kuchukua hatua zipi ili kuzuia hali hii?

   **(Mwanafunzi ajibu)**

3. Unadhani kutatokea nini jamii yako isipozuia kuenea kwa magonjwa yanayoambukizwa?

   **(Mwanafunzi ajibu)**

4. Ukambi ni ugonjwa wa kuambukizwa. Jina jingine la ukambi ni _______

   **(Mwanafunzi ajibu)**

**Geuza ukurasa**



@ KNEC 2024

**(II) UFAHAMU WA KUSIKILIZA**

**Maagizo maalum**

i. *Msomee mwanafunzi kifungu kifuatacho **mara mbili.***

ii. *Mjulishe kuwa atajibu maswali baada ya kusomewa kifungu mara ya pili.*

Guru alikuwa kijana mwenye umri wa miaka kumi na mitatu. Alisomea katika shule ya Tusonge. Aliyekutana na kijana huyu alipojiunga na shule hii, asingewazia kuwa angekuwa mwimbaji wa kutajika katika eneo zima la Buraha. Waulize wenzake waliokutana naye siku hizo. Watakwambia kwamba mja huyu alizungumza kwa sauti hafifu kabisa. Ilikuwa vigumu kumsikia ukiwa karibu naye.

Udhaifu wa sauti ya Guru ulikuwa kama chura kwenye maji. Kamwe haukumzuia kukitambua na kukiendeleza kipaji chake cha uimbaji. Polepole aliitia makali sauti yake, nayo haikumkaidi. Iliimarika, ikawa kama ya ninga. Guru hakuchelea kuitumia sauti hii kuwatumbuiza wengi; shuleni na nje ya shule. Haikuwa ibra kumwona akiwaongoza wenzake kwenye gwaride; kuimba nyimbo ambazo alikuwa amezitunga mwenyewe. Nyimbo hizi zilihusu masuala mbalimbali yanayoiathiri jamii.

Sifa za Guru zilienea kama moto nyikani. Alipata mialiko kuwaelimisha wanajamii kwa nyimbo mbalimbali. Kilele cha ufanisi wake kilikuwa mwaliko alioupokea kutoka Ikulu ya Taifa. Hapo yeye na wenzake walipata fursa ya kuwatumbuiza maelfu ya raia waliohudhuria sherehe ya kuadhimisha Siku ya Mashujaa. Lililomtia fahari zaidi ni nafasi ya kumwamkua rais kwa viganja vyake mwenyewe. Hangeweza kuficha fahari hii hata kwa mwalimu mlezi wao ambaye alikuwa ameandamana nao.

5. Guru alisomea shule gani?

   **(Mwanafunzi ajibu)**

6. Ni jambo gani katika kifungu linaloonyesha kwamba Guru anajiamini?

   **(Mwanafunzi ajibu)**

7. Unadhani kulitokea nini baada ya Guru kuwasilisha wimbo kwenye ikulu?

   **(Mwanafunzi ajibu)**

8. Kulingana na kifungu maana ya **kutia makali ni**?

   **( Mwanafunzi ajibu)**



@ KNEC 2024

**ZOEZI 2 : KUSOMA KWA SAUTI**

**Maagizo maalum**

i. *Mfahamishe mwanafunzi matarajio ya Zoezi la Kusoma. (Zingatia mwongozo wa kutathminia Kusoma kwa sauti).*

ii. *Mpe mwanafunzi nakala atakayoisoma kwa sauti.*

iii. *Mwanafunzi anaposoma, sikiliza na kurekodi idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa **dakika moja.***

iv. *Onyesha kwa mshazari **(/)** mahali mwanafunzi alipofikia kusoma **dakika moja** ikikamilika.*

v. *Mruhusu mwanafunzi kusoma kifungu mpaka mwisho.*

vi. *Pigia mstari maneno **yote** ambayo mwanafunzi atashindwa kuyasoma au kuyatamka vizuri.*

vii. *Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi ameweza **kusoma kwa usahihi** kwa dakika **moja**. (Baada ya kuondoa yaliyotamkwa vibaya au/na aliyoshindwa kutamka)*

viii. *Rekodi viwango vya umilisi wa mwanafunzi kwa kuzingatia mwongozo uliopewa.*

ix. *Hakikisha una nakala ya kurekodia tathmini hii. (Iwe na majina ya wanafunzi wote.)*

x. *Ukiwa tayari kuanza tathmini, sema,*

‘‘Sasa naomba unisomee kifungu hiki kwa sauti.’’

## Mwalimu amwambie mwanafunzi asome kifungu kifuatacho kwa sauti.

Je, umewahi kuwaza kuhusu jinsi ambavyo jamii ingekuwa iwapo kila[10] mtu angekosa maadili ya kibinafsi? Fikiria kwa mfano, unataka kuingia[20] darasani, naye mwenzako amesimama mlangoni, hataki kukupisha. Utahisi vipi? Bila[30] shaka utaudhika.Utamwambia, “Simile!” Hapo utakuwa umemwomba akupe nafasi upite[40]. Huenda hata ukatumia mfano wa huyo mwenzako kuwafunza wengine kuhusu[50] umuhimu wa maadili ya mtu binfasi. Utawaambia kwamba mtu huanza[60] kujifunza maadili akiwa mchanga. Lau sivyo itakuwa vigumu kuyapata. Bila[70] shaka unafahamu kwamba samaki hukunjwa angali mbichi.

Yakini, maadili ya[80] mtu binafsi ni nguzo kuu katika kujenga mshikamano wa kijamii[90]. Matendo madogomadogo ya kimaadili kama[95] vile kuamkua wengine, kushukuru kwa mema, kuyaheshimu maoni ya wengine, na kuwahi shughuli muhimu, hupalilia mahusiano mema.



@ KNEC 2024